TANGAZO LA SERIKALI NA 943 la tarehe 29/11/2019

SHERIA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA,
(NA. 5 YA MWAKA 2019)

AGIZO

(Imetolewa kwa mujibu wa Kifungu Na.29(1) (d))

AGIZO LA MAREKEBISHO YA BEI YA MAMLAKA YA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA MPANDA (MPANDA WSSA), 2019

Jina la Agizo

1. Agizo hili litajulikana kama, Agizo la Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mpanda(“Mpanda WSSA”),(Kurekebisha Bei za Huduma za Maji safi), la Mwaka 2019.

Tarehe ya Kuanza

2. Agizo hili litaanza kutekelezwa rasmi kuanzia tarehe 1 Disemba 2019.

Marekebisho ya Bei

3. Bei za majisafi na usafi wa mazingira za Mpanda WSSA zinarekebishwa kulingana na Jedwali la Kwanza katika Agizo hili.

Masharti

4. Bei zilizoidhinishwa zitaambatana na masharti yafuatayo:

(a) kabla ya kuanza kutekeleza bei mpya, Mpanda WSSA iwasilishe EWURA vielelezo kwamba ilitoa taarifa kwa wateja wake kuhusu bei mpya za huduma zake na pia ilitoa elimu kikamilifu kwa umma ikiwa ni pamoja na wawakilishi wa wananchi, serikali na viongozi wa dini katika eneo lake la huduma;

(b) kabla au Ifikapo tarehe 30 Juni 2020, Mpanda WSSA ihakikishe imetafuta na kutenga eneo kwa ajili ya kumwaga maji taka;

(c) Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mpanda, kwa kutumia mapato yatokanayo na bei zilizoidhinishwa, itatekeleza miradi iliyoainishwa katika Jedwali la Pili la Agizo hili;

(d) Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mpanda itafikia viashiria vya utendaji kama ilivyooneshwa kwenye Jedwali la Tatu la Agizo hili;

(e) Ifikapo tarehe 31 Disemba 2019 au kabla, Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mpanda itawasilisha EWURA Mpango wake wa Kibiashara uliopitiwa upya kwa kuzingatia bei zilizoidhinishwa na mpango wa utekelezaji wa masharti ya Agizo hili;

(f) Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mpanda ihakikishe kuwa inazingatia matakwa ya kukusanya tozo ya udhibiti na kuiwasilisha EWURA kama ilivyobainishwa katika kifungu cha 43 cha Sheria ya EWURA Sura ya 414 na Kanuni ya 6 ya Kanuni za EWURA (Utaratibu wa Kukusanya Tozo) zilizotolewa kwenye Tangazo la Serikali la mwaka 2010;

Sura ya 414

T. S. Na. 193 la mwaka 2010

(g) Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mpanda ihakikishe vitabu vyake vya fedha vinakaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali au mtu yeyote aliyeidhinishwa kulingana na kifungu 33(1) cha Sheria ya Ukaguzi wa Mahesabu ya Umma na kuwasilisha nakala za mahesabu yaliyokaguliwa EWURA;

Cap. 348

(h) Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mpanda ihakikishe inafungia wateja wote wa majumbani dira ifikapo tarehe 31 Januari 2020;

(i) Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mpanda, kwa kila mwaka kama sehemu ya taarifa yake ya utendaji ya mwaka, itawasilisha taarifa ya utekelezaji wa masharti yaliyopo kwenye Agizo la Bei na kila kifungu cha

gharama katika mahitaji ya fedha yaliyoidhinishwa kama yalivyoainishwa katika Jedwali la Nne; na

(j) Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mpanda itaendelea kuwasilisha EWURA taarifa zake za fedha na utendaji kwa mujibu wa matakwa ya EWURA. Taarifa hizi zitatumiwa na EWURA katika kufanya tathmini ya utendaji wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mpanda ikilinganishwa na Mamlaka nyingine za Majisafi na Usafi wa Mazingira na uboreshaji wa huduma zake. Pia EWURA itazingatia tathmini hii katika kufanya maamuzi ya maombi yote yatakayowasilishwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mpanda katika siku zijazo.

.

Utenguzi wa Agizo Na. 2016 -005 la 29 Januari 2016

5. Agizo la Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mpanda(“Mpanda WSSA”),(la Bei za Huduma za Maji safi), la Mwaka, 2016 linatenguliwa.

MAJEDWALI

JEDWALI LA KWANZA

(Limetengenezwa chini ya aya ya 3)

BEI NA ADA ZILIZOIDHINISHWA

Jedwali Namba 1(a): Bei za Maji za Sasa na Zilizoidhinishwa kwa Wateja Wenye Dira (Shilingi/ Mita ya Ujazo)

Kundi la Wateja	Bei za Sasa	Bei Zinazopendekezwa			Bei Zilizoidhinishwa		
	2018/19	2019/20	2020/21	2021/22	2019/20	2020/21	2021/22
Majumbani							
Kundi la Kwanza (1-5uniti)	950	1,200	1,300	1,300	1,100	1,200	1,300
Kundi la Pili(>5uniti)	950	1,600	1,800	1,800	1,100	1,250	1,400
Taasisi	1,020	1,700	1,790	1,810	1,200	1,350	1,500
Biashara	1,050	1,700	1,840	1,860	1,250	1,400	1,550
Viwanda	1,200	1,930	2,100	2,130	1,400	1,600	1,750
Magati	1,000	1,000	1,000	1,000	1,000	1,000	1,000
WastaniwaUlinganisho	976	1,560	1,684	1,689	1,113	1,236	1,359

Jedwali Namba 1(b): Bei za Maji za Sasa na Zilizoidhinishwa kwa Wateja Wasio na Dira (Shilingi/ Mwezi)

<table>
<tr><td rowspan="2">Kundi la Wateja</td><td>Bei za Sasa</td><td colspan="3">Bei Zinazopendekezwa</td><td colspan="2">Bei Zilizoidhinishwa</td></tr>
<tr><td>2018/19</td><td>2019/20</td><td>2020/21</td><td>2021/22</td><td>2019/20</td><td>2020/21 – 2021/22</td></tr>
<tr><td>Majumbani</td><td>14,000</td><td>26,400</td><td colspan="2" rowspan="5">Mpanda itahakikishakuwa watejawotewamefungiwadira</td><td>16,100</td><td rowspan="5">Beizawatejawasionadirahaziruhusiwikwawatejawote</td></tr>
<tr><td>Taasisi</td><td colspan="2" rowspan="4">Watejawotekatikahayamakundiwamewekewadira</td><td rowspan="4">Beizawatejawasionadirahaziruhusiwikwawatejawasiowamajumbani</td></tr>
<tr><td>Biashara</td></tr>
<tr><td>Viwanda</td></tr>
<tr><td>Magati</td></tr>
</table>

Ada ya Sasa na Iliyoidhinishwa ya Maunganisho ya Maji Safi (Shilingi/Maunganisho)

Kundi la Wateja	**Ada ya Sasa**	**Ada Iliyopendekezwa**	**Ada Iliyoidhinishwa**
	2018/19	**2019/20 – 2021/22**	**2019/20 – 2021/22**
Wateja Wote	**Asilimia ishirini ya gharama za maunganisho kama inavyojieleza katika Kifungu cha 24 cha Kanuni za Maji za 2013**	**Asilimia ishirini ya gharama za maunganisho kama inavyojieleza katika Kifungu cha 24 cha Kanuni za Maji za 2013**	**Asilimia ishirini ya gharama za maunganisho kama inavyojieleza katika Kifungu cha 24 cha Kanuni za Maji za 2013**

Jedwali Namba 1(c): Ada ya Sasa na Iliyoidhinishwa ya Kurejeshewa Huduma ya Maji Baada ya Kukatiwa (Shilingi/Kurejeshewa Huduma)

Kundi la Wateja	Ada za Sasa	Ada Zilizopendekezwa			Ada Zilizoidhinishwa		
	2018/19	2019/2	2020/2	2021/2	2019/2	2020/2	2021/22
Majumbani	15,000	25,800	26,728	27,691	15,000	15,000	15,000
Taasisi	15,000	48,000	49,728	51,518	15,000	15,000	15,000
Biashara	15,000	48,000	49,728	51,518	15,000	15,000	15,000
Viwanda	15,000	373,20	386,63	400,55	15,000	15,000	15,000
Magati	15,000	48,000	49,728	51,518	15,000	15,000	15,000

JEDWALI LA PILI

(Limetengenezwa chini ya aya ya 4(c))

MIRADI ITAKAYOTEKELEZWA

Maelezo ya Kazi				**Mwisho wa Utekelezaji**
	2019/20	**2020/21**	**2021/22**	
UkarabatinaKubadilisha Mali				
Kubadilishaball valvu7 (zaainayabrass material) katikamatanki 7	**14**			**Julai 2020**

Maelezo ya Kazi				**Mwisho wa Utekelezaji**
	2019/20	**2020/21**	**2021/22**	
Kubadilidira 10 kubwazamajimaeneoyaMangaBPT, Kigamboni, tanki la Kazima,tanki la ShanwenaMilala. Dirambilizitabadilishwamwakawa kwanza nadira 8 mwakawatatu.	**4**		**17.64**	**Julai 2020, &Julai 2021**
Kubadilishadirazawateja1500 (1000 mwakawa pili na 500 mwakawatatu)		**126**	**66.15**	**Julai 2021 & 20222**
Kubadilishapampumbilizamajikatikakisima cha Ikulu (uwezowaumemewa unit 4.5) napampukatikakisima cha Majengo (uwezowaumemewauniti 5).	**18**		**20**	**Julai 2020 &Julai 2022**
UwekezajiMpya				
KujengamradiwaKanoge II wamsererekokutokaKanogekwendaTanki la Kazimanakukununuamabombayenyekipenyo cha 8na viungiovyakekwaurefuwakilomita 12			**515**	**Julai 2022**
Kuongezamtandaowamajikatikamaeneoambayohayanamtandaomaeneoya Tulieni, Kawalyowa (5km), Mtapenda (0.5km), Kazima (3km), Rungwa 1km, Misengeleni 4km, Misunkumilo (1km), Mapinduzi (3km), Kilimahewa (2km), Nsemulwa (1km) and Makanyagio (0.5km)			**327.57**	**Julai 2022**
Kununuadira 1,200 zawatejawasionadirapamojanaviounggiovyake	**144**			**Julai 2020**
Kununuadira 12000 pamojanaviungiovyake ,dira 400 kilamwakakwaajiliyawatejawapya.	**48**	**50**	**53**	**Julai 2020,2021, 2022**
Kununuaardhikwaajiliyakumwaganakuti bumaji taka	**12**			**Julai 2020**
Jumla ya Gharama za Uwekezaji	**222**	**176**	**999.28**	

JEDWALI LA TATU

(Limetengenezwa chini ya aya ya 4(d))

VIASHIRIA VYA UTENDAJI

	Utendaji wa sasa	Malengo ya Viashiriavya Utendaji		
Kiashiria	2018/19	2019/20	2020/21	2021/22
NambayaWatejaWapya		400	400	400
UwianowaKufungaDira (%)	87	100	100	100
UpotevuwaMaji	28%	28%	26%	25%
MasaayaKutoaHuduma	6	8	12	14
UfanisikatikaUkusanyajiMapato	88%	90%	92%	95%

JEDWALI LA NNE

(Limetengenezwa chini ya aya ya 4(i))

MAHITAJI YA FEDHA YALIYOIDHINISHWA (SHILINGI KWA MILIONI)

Gharama/ Maelezo	2019/20		2020/21		2021/22	
	Iliyopendekezwa	Iliyoidhinishwa	Iliyopendekezwa	Iliyoidhinishwa	Iliyopendekezwa	Iliyoidhinishwa
Uzalishaji	34.50	15.31	41.00	15.71	42.00	21.87
UmemekwaajiliyaUzalishaji	35.50	30.50	40.00	30.50	40.00	54.71
Usambaji	9.00	8.40	11.00	8.82	42.00	39.26
Matengenezo	25.00	72.80	25.00	80.00	30.00	84.90
Watumishi	423.90	284.22	430.50	430.38	445.90	571.27
Utawala	323.40	263.56	337.30	283.79	342.80	304.34
Matangazo	0.00	4.70	0.00	4.94	0.00	5.18
Matukio	19.50	15.18	20.00	15.88	24.00	16.63
Fedha	5.00	4.20	6.00	4.41	6.00	4.63
Jumla ya Gharama za Uendeshaji na Matengenezo	875.80	698.86	910.80	874.43	972.70	1,102.80
Uchakavu	194.60	224.30	196.50	229.39	0.00	398.61
Uwekezaji	0	24.23	0	330.79	0	402.84
Mahitaji Yote ya Fedha	1,070.40	947.38	1,107.30	1,434.61	972.70	1,904.25

Gharama/ Maelezo	2019/20		2020/21		2021/22	
	Iliyopendekezwa	Iliyoidhinishwa	Iliyopendekezwa	Iliyoidhinishwa	Iliyopendekezwa	Iliyoidhinishwa
KuondoaMapatoMengine	42.60	42.60	42.60	42.60	43.60	43.60
Mahitaji ya Fedha Yanayotokana na Huduma ya Maji	1,027.80	904.78	1,064.70	1,392.01	929.10	1,860.65

Dodoma
14 Novemba, 2019

NZINYANGWA E. MCHANY
Mkurugenzi Mkuu